JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

Namba za Simu…………………..
Mkuu wa Shule 0620261208
Makamu Mkuu wa Shule 0625870498
Matron 0624082394
Shule ya Sekondari Ndolwa
S.L.P 262 HANDENI

Tarehe 12/06/2023

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….
…………………………………………..
S.L.P …………………………………..
………………………………………….

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NDOLWA HALMASHAURI YA HANDENI MKOA TANGA MWAKA 2023.

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya PCB/HGE

   Shule ya Sekondari NDOLWA ipo umbali wa Kilometa 12 Kutoka barabara kuu ya Tanga-Dar es- Salaam Wilaya ya Handeni,Tarafa ya Mzundu,Kata ya Ndolwa,Kijiji cha Mzundu.Mwanafunzi anapaswa kushuka kituo cha KWEDIKWAZU kilichopo barabara kuu ya Tanga-Dar es salaam.Usafiri wa bodaboda unapatikana kwa shilingi elfu sita (6000/=) mpaka shuleni.Kama unatokea Tanga mjini panda basi la Satco linaloenda kwamkono utashuka shuleni nauli ni elfu saba (7000/=) kutoka Tanga mjini hadi shuleni.

   Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14/08/2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2023.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili dark blue kwa Wasichana mshono ni linda box iliyovuka magoti.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.

iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni rangi nyeupe.ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni tshirt nyekundu na suruali ya track nyekundu na Raba nyeupe au nyeusi.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi pea mbili.
vi. Soksi jozi mbili nyeupe.
vii. Skafu dark blue
viii. Sweta rangi ya bluu.
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) magauni mawili ya pinki.
x. Tisheti (T-shirt) rangi ya karoti inapatikana shuleni.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa 10,kalamu za kutosha na Mathematical set.
ii. Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (PCB au HGE)
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator(fx991)
vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya inchi mbili na nusu.
vii. Mashuka Jozi 2 na foronya ya godoro 1 rangi ya Pink, chandarua 1.
viii. Nguo za ndani za kutosha,Taulo,ndala,mswaki,kanga/vitenge viwili,mto,nguo ya kulalia na mahitaji mengine ya mtoto wa kike.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, Jembe lenye mpini 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
xii. Sanduku la bati la kuhifadhia vitu vyake.

2.3 Michango mbalimbali

a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Fedha hii ilipwe kwenye akaunti ya shule 4141200053 Jina la Akaunti ni NDOLWA SEKONDARI,mwanafunzi aje na bank pay in slip.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu

nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule …. [signature]

Jina la Mkuu wa Shule; NOEL E.KIMARO

Mhuri wa Mkuu wa Shule ….. Headmaster Ndolwa Sec. School Box 262 Handeni

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO

USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- ➢ Mkuu wa shule;0620261208
- ➢ Makamu Mkuu wa Shule;0625870498
- ➢ Mwandamizi Taaluma;0625680981
- ➢ Mwandamizi Malezi;0687555517

PRESIDENT OFFICE
LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMISTRATION
HANDENI DISTRICT COUNCIL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

NDOLWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 262
HANDENI

DATE…………………………………….

MEDICAL OFFICER
……………................……… GOVERNMENT HOSPITAL
……………………………………………………………………
…………………………………………………………………….

NAME OF PUPIL ……………………………………………………………………………………………………………

Please examine the above named girl to ascertain her fitness for further education

.....................………………
HEAD OF SCHOOL

MEDICAL CERTIFICATE
(To be completed by the medical officer)

I have examined the above named with regard to:

SKIN………………………………………………………………………………………………………………………

EYES……………………………………………………………………………………………………………………….

EARS………………………………………………………………………………………………………………………

CHEST…………………………………………………………………………………………………………………….

SPLEEN…………………………………………………………………………………………………………………..

ABDOMEN………………………………………………………………………………………………………………

URINE…………………………………………………………………………………………………………………….

STOOL……………………………………………………………………………………………………………………

HEMOGLOBIN………………………………………………………………………………………………………….

And I considered :

1.She has good health, free from infection diseases worms, bilharzias and fit to go school

2.She is now fit to return to school having treatment for……………………………………………

3.She is now fit to return/Join to school having checked for…………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………..............……………………        ………………………………………………………

NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER        DATE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI MITAA

HALMASHAURI YA HANDENI

NDOLWA SEKONDARI

S.L.P 262

HANDENI

FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA

SEHEMU A:Taarifa za mwanafunzi

1.jina kamili……………………………………………………………………………………………………

2.Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………………………………………………..

3.Wilaya alipozaliwa……………………………………………………Mji/kijiji…………………………………..

4.Kukubali nafasi (ijazwe na mwanafunzi)

Mimi…………………………………………………………………………..nimeona maagizo yote ya kujiunga na shule ya sekondari Ndolwa na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule.Nitapokuwa shuleni Ndolwa nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata elimu.

Sahihi ya mwanafunzi………………………………………………………tarehe…………………………………..

**SEHEMU B:Habari za mzazi /mlezi (ijazwe na mzazi/mlezi)**

1.Jina kamili……………………………………………………………………………………………………

2.Yeye ni mzazi/mlezi………………………………………………………………………………………..

3.Kazi yake……………………………………………………………………………………………………..

4.Anwani ya mzazi/mlezi

……………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………….

5.Namba tatu za simu ikiwemo ya mzazi /mlezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi

(a)……………………………………………………………………………….

(b)……………………………………………………………………………….

(c)……………………………………………………………………………….

**UTHIBITISHO**

Mimi mzazi/mlezi wa ………………………………………………………………………….nimehakikisha kwamba maagizo yote yameeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A.

Sahihi ya Mzazi /mlezi…………………………………………………Tarehe…………………………………………….